JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kotra" Nyerere Road,
S.L.P. 377,
MUSOMA,
Barua Pepe: rbcmara@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

MUSOMA, MARA – JULAI 28, 2022

WANANCHI MKOA WA MARA WAPATA ELIMU YA RUSHWA NA KUFURAHISHWA NA FILAMU ZA BAHASHA NA 'THE ROYAL TOUR'

Ndugu Wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Aprili hadi Juni, 2022 ambapo mkazo uliwekwa katika kuongeza nguvu zaidi kwenye **kuzuia vitendo vya rushwa.** Hii ilifanyika kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji wa taarifa ili kubaini vitendo vya rushwa kabla havijafanyika na pia kuchukuwa hatua kali za kisheria kwa wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Vilevile kwa kufanya uelimishaji wa jamii hususani kupitia ushirikiano kati ya TAKUKURU na Chama cha Skauti nchini kupitia Mpango unaojulikana kama TAKUSKA, unaolenga kuwafikia vijana wengi zaidi katika mkoa wetu.

Uelimishaji Umma:

NA.	KAZI	UFAFANUZI
1	Kutembelea na kuziimarisha Klabu za Wapinga rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo	Klabu za Wapinga rushwa zipatazo 86 zimetembelewa katika wilaya zote za Mkoa wa Mara na kumekuwa na mwamko wa vijana katika kupinga rushwa na kukuza maadili ya Kitanzania ya kuzingatia haki na usawa
2	Kutembelea Wananchi katika Vitongoji, Mitaa na	Jumla ya Mikutano 30 ya Hadhara ilifanyika katika maeneo mbalimbali ndani ya mkoa

	Vijiji kwa lengo la kufanya Mikutano ya Hadhara	
3	Kufanya Semina katika Vikao mbalimbali	Kwa nyakati tofauti tumeshiriki katika vikao 15 na kutoa mada mbalimbali za kuelimisha Umma juu ya rushwa na madhara yake katika Jamii
4	Kushiriki katika vipindi vya Redio	Tumeshiriki katika vipindi 3 vya redio katika vituo vya Victoria Fm, Mazingira Fm na Bunda Fm
5	Kushiriki katika TAKUKURU Inayotembea	Kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Butiama tulifanya kikao na Viongozi wa AMCOS na Wanachama wao kutatua migogoro eneo la viwanja vya Shule ya Msingi Butiama 'B'
6	Kushiriki katika Maonesho kwenye sherehe ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere	Tulishiriki jumla ya Maonesho 9 mojawapo likiwa ni sherehe ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mnamo Tarehe 13/4/2022 katika Viwanja vya Mwenge wilayani Butiama
7	Kushiriki na kutoa elimu juu ya rushwa katika Mbio za Mwenge wa Uhuru kupitia Filamu (Sinema)	Kuanzia tarehe 27/6/2022 hadi 30/6/2022 katika Wilaya za Serengeti, Tarime na Rorya tulishiriki kutoa elimu kwa njia ya Filamu ya Bahasha inayotoa mafunzo juu ya madhara ya rushwa na 'Royal Tour' ambapo jumla ya wananchi 3,807 wanakadiriwa kuangalia Filamu hizi mbili.
8	Kutoa Semina kwa Wadau wa Sekta ya Afya kwa Halmashauri za Wilaya za Musoma na Bunda	TAKUKURU Mkoa wa Mara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali – SIKIKA tulitoa Semina kwa Wadau wa Sekta ya Afya 50 kwa Halmashauri za Wilaya za Musoma na Bunda kuanzia tarehe 24/5/2022 hadi 27/5/2022. Semina hii ilihusisha wawakilishi wa kutoka makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Makatibu wa Afya Wilaya, Kamati za Afya kutoka Vituo vya kutolea Huduma za Afya, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wilaya, Madiwani, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji, Watu wenye ulemavu na kundi la

		Vijana. Mafunzo haya yalikusudia kufikisha ujumbe katika jamii juu ya ushiriki wa jamii katika kufuatilia matumizi ya fedha za umma hasa kwenye Sekta ya Afya na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao ya **TAKUKURU**

UZUIAJI RUSHWA:

Kwa kuzingatia kwamba Miradi ya Maendeleo ni mali ya Wananchi na kwamba Serikali inapeleka fedha nyingi katika eneo hilo, TAKUKURU Mkoa wa Mara imefuatilia utekelezaji wa **Miradi 24** yenye thamani ya Shillingi Billioni Kumi na Nane Millioni Mia Tano Sabini na Nane, Laki Tatu na Elfu Tisa, Mia Nne Themanini na Tano **(Shs. 18,578,309,485)** katika Sekta za Afya, Barabara, Maji na Elimu. Miradi mitatu (3) ilibainika kuwa na changamoto kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa ujenzi wa Chumba cha Wagonjwa wa Dharura Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime katika Sekta ya Afya thamani yake ikiwa ni shs. 300,000,000/=. Mradi huu ulichelewa kuanza kutekelezwa na baada ya ufuatiliaji wa karibu, ujenzi sasa unaendelea vizuri.

(ii) Mradi wa Maji katika Kijiji cha Robanda Wilaya ya Serengeti wenye thamani ya shs. 685,151,776. Katika ufuatiliaji wake, upungufu uliobainika ni ukiukwaji wa Sheria na Taratibu za Manunuzi na uchunguzi umeanzishwa.

(iii) Mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa - shule ya sekondari ya Mapinduzi wilayani Serengeti, wenye thamani ya shs. 120,000,000/=, Mapungufu yaliyobainika ni Upigaji wa Rangi kwenye madarasa hauna ubora na 'scheeming' hazijafanyika. Pia Ubao wa kuandikia kukosa sehemu ya kuweka ufutio kwa Mwalimu, Ubao kupinda pande na Vitasa vya milango kukosa ubora. Walielekezwa kufanya marekebisho na ufuatiliaji unaendelea ili kuhakikisha kuwa marekebisho stahiki yanafanyika.

UCHAMBUZI WA MIFUMO NA WARSHA

Ndugu Wanahabari,

TAKUKURU mkoa wa Mara, imefanya **Uchambuzi mbili (2) wa mfumo** katika Sekta mbalimbali pamoja na **Warsha mbili (2)** za wadau kama ifuatayo;

1. **Mfumo wa ukusanyaji wa mapato** yanayotokana na ushuru wa madini ya ujenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.
   Katika uchambuzi huo, yapo mapungufu yaliyobainika ambayo ni pamoja na mwitikio mdogo wa ukataji wa leseni pamoja na changamoto katika ukusanyaji wa taarifa za kiasi cha madini ya ujenzi, kilichochimbwa ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kufanya udanganyifu.

   Katika kikao cha Warsha tulikubaliana kuwa Halmashauri iyatambue maeneo yanakopatikana madini mbalimbali ya ujenzi ili kurahisisha ufuatiliaji na ukusanyaji wa mapato. Aidha tulikubaliana pia kuwa Halmashauri iwasiliane na Taasisi kama vile TANROADS na TARURA ili kupata kiasi cha madini ambacho wakandarasi wanahitaji ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mahitaji ya madini ya ujenzi kama vile kifusi, mawe pamoja na mchanga, hivyo kupata taarifa sahihi na kuboresha mapato yanayotokana na ushuru wa madini ya ujenzi.

2. **Mfumo wa utendaji kazi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Ununuzi wa Umma (GPSA).** Katika uchambuzi huo yapo mapungufu mbalimbali yaliyobainika, ikiwa ni pamoja na wateja wengi kwa maana ya Taasisi za Serikali, kutoridhishwa na huduma za GPSA. Aidha ilibainika pia kuwa wananchi wengi hawafahamu huduma zinazotolewa na Wakala huyo, ikiwemo kazi ya ugomboaji wa mizigo bandarini, viwanja vya ndege na mipakani.

   - Ilifanyika warsha ya wadau wa mfumo wa upatikanaji wa taarifa za mahitaji ya miundombinu ya elimu, ikiwa ni pamoja na vyumba vya madarasa na madawati. Katika warsha hiyo, wadau walikubaliana kuwa idara za Elimu Msingi na Sekondari,

zishirikiane katika kufanya maoteo ya wanafunzi watakojiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka unaofuata. Aidha walikubaliana pia kuwa wadau mbalimbali, zikiwemo Taasisi za fedha na makampuni ya simu, zishirikishwe katika kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa pamoja na madawati.

- Ilifanyika pia Warsha ya wadau wa mfumo wa usimamizi wa mitihani katika vyuo vya kati vinavyosimamiwa na NACTE. Katika Warsha hiyo wadau walikubaliana kuwa sheria na taratibu za mitihani zizingatiwe kwa maana ya kufanyia mitihani 'moderation' na matokeo ya mitihani yawe yanatolewa mapema

UCHUNGUZI

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha Aprili – Juni, 2022 jumla ya malalamiko **106** yalipokelewa. Kati ya hayo malalamiko **79** yalihusu vitendo vya rushwa na **27** hayakuhusisha vitendo vya Rushwa. Kutokana na malalamiko **27** ambayo hayakuhusu rushwa, walalamikaji walipatiwa ushauri, kuelimishwa na mengine 5 yalihamishiwa Idara zingine kwa kupatiwa ufumbuzi. Malalamiko haya **79** yanayohusu rushwa yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kukusanya nyaraka za ushahidi, kuwahoji mashahidi na watuhumiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Katika kipindi tajwa uchunguzi wa majalada 18 ulikamilika, kesi 18 zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi zinazoendelea Mahakamani mpaka sasa kuwa 36. Kesi 3 ziliamuliwa Mahakamani ambapo kesi 2 washitakiwa walipatikana na hatia na kesi 1 mshitakiwa aliachiwa huru.

Mchanganuo wa kisekta wa malalamiko **79** yaliyopokelewa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo-:

SN	IDARA/SEKTA	IDADI
1	Ushirika	1

2	Binafsi	3
3	Polisi	7
4	Elimu	4
5	Mahakama	3
6	TAMISEMI	26
7	Siasa	1
8	Afya	11
9	TARURA	1
10	Utalii	1
11	Ardhi	6
12	Maji	4
13	Fedha	6
14	Uvuvi	1
15	TANESCO	2
16	Madini	1
17	RITA	1
	JUMLA	**79**

MIKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI– SEPTEMBA, 2022

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha Julai – Septemba, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mara tunatarajia kuongeza nguvu zaidi kwenye **Kuzuia Vitendo vya rushwa** kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji habari ili kubaini vitendo vya rushwa kabla havijafanyika, lakini pia kuchukuwa hatua kali za kisheria kwa wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa

Vilevile, kwa kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Mara itafanya uelimishaji wa jamii hususan kupitia ushirikiano kati ya TAKUKURU na Chama cha Skauti nchini kupitia Mpango unaojulikana kama TAKUSKA, unaolenga kuwafikia vijana wengi zaidi katika mkoa wetu.

WITO:

Ndugu Wanahabari,

Mwisho natoa shukrani kwenu Wanahabari kwa ushirikiano wenu mkubwa katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

WITO:

Ndugu Wanahabari,

Mwisho natoa shukrani kwenu Wanahabari kwa ushirikiano wenu mkubwa katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Mara inatoa wito kwa jamii ya wana-Mara kwa ujumla kutokujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

Tunawasihi wananchi wote wa Mkoa wa Mara kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 au kupiga simu ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa ambayo ni **0738-150130** au kufika katika ofisi za TAKUKURU iliyo karibu nawe.

Kwa pamoja tushirikiane kuitokomeza rushwa

TANZANIA BILA RUSHWA INAWEZEKANA NA KAZI IENDELEE

Imetolewana: **Imetolewa na:**

ANTHONY GANG'OLO
Naibu Mkuu wa TAKUKURU (M) Mara
Simu: 0738150131

Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022